BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

70 Barabara ya Chukuwani, Buyu
70490 Mjini Magharibi,
S. L. P 902 Chukwani,
Zanzibar, Tanzania

Simu: +255 24 224 2000
Nukushi: +255 24 224 2000
info@zanzibarassembly.go.tz
www.zanzibarassembly.go.tz

# HOTUBA YA MAONI YA KAMATI YA USTAWI WA JAMII KUHUSU MAKADIRIO YA MAPATO NA MATUMIZI YA WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,**

Nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu mwingi wa rehema, kwa kutujaalia uzima na afya njema tukaweza kukutana tena katika Baraza hili la Kumi kwa ajili ya kuendelea kuwatumikia wananchi wetu. Aidha, nikushukuru na kukupongeza wewe Mheshimiwa Spika kwa kuliongoza Baraza hili tukufu, ni imani yetu kwamba utaendelea kuliongoza Baraza hili kwa uadilifu wa hali ya juu na kuimarisha Demokrasia katika chombo hichi muhimu cha wananchi.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa upekee kabisa, nichukue fursa hii kumpongeza Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Hussein Ali Hassan Mwinyi kwa kutuletea maendeleo nchini pamoja na wasaidizi wake Makamu wa Kwanza wa Rais Mhe. Othman Masoud Othman na Makamu wa Pili Mhe. Hemed Suleiman Abdulla kwa kumsaidia vyema Mhe. Rais wetu katika kutekeleza majukumu yake.

**Mheshimiwa Spika,**

Vile vile, Naomba niwakumbushe wajumbe wenzangu kuwa kipindi chetu cha miaka mitano kinakimbia kwa kasi kubwa, hivyo kila mmoja wetu ajitahidi kutekeleza aliyoyaahidi na kwa pamoja tutakuwa tumemsaidia Mheshimiwa Rais kutekeleza Ilani ya Chama cha Mapinduzi na kukamilisha ahadi kwa wananchi waliotuchagua kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,**

Sina budi pia kumshukuru Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto pamoja na Katibu Mkuu, Naibu Katibu Mkuu, Afisa Mdhamini, Wakurugenzi na watendaji wote wa Wizara hii kwa mashirikiano waliyotupatia wakati wa kupitia Makadirio ya Bajeti ya Wizara yao.

Pia nichukue nafasi hii kuwashukuru Wajumbe wa Kamati yetu kwa umoja wao na kazi nzuri waliyoifanya kiasi cha kunirahisishia kazi ya kuongoza kikao kuwa nyepesi na ya ufanisi.

Kwa kweli, ni wajumbe Mahiri, ambao wameweza kuyajadili kwa kina na ipasavyo makadirio hayo na kuhoji mambo mbali mbali kwa lengo la kuhakikisha kwamba fedha wanazoidhinisha zinatumiwa kwa matumizi yaliokusudiwa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa heshima ya hali ya juu napenda kuwatambua Wajumbe hao kwa majina kama hivi ifuatavyo:-

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Mhe. Sabiha Filfil Thani | Mwenyekiti |
| 2. | Mhe. Nassor Salim Ali (Jazira) | Makamu Mwenyekiti |
| 3. | Mhe. Abdulla Hussein Kombo | Mjumbe |
| 4. | Mhe. Haji Omar Kheri | Mjumbe |
| 5. | Mhe. Sulubu Kidongo Amour | Mjumbe |
| 6. | Mhe. Bihindi Hamad Khamis | Mjumbe |
| 7. | Mhe. Salma Mussa Bilal | Mjumbe |
| 8. | Mhe. Bahati Khamis Kombo | Mjumbe |

Aidha, Kamati yetu inafanyakazi na makatibu watatu (3) ambao kwa kiasi kikubwa wamekuwa wakitusaidia sana katika kutekeleza majukumu yetu, makatibu hao ni:

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Ndg. Bakar Makame Haji | Katibu |
| 2. | Ndg. Talib Enzi Talib | Katibu |
| 3. | Ndg. Salha Abdulla Abdulla | Katibu |

**Mheshimiwa Spika,**

Miongoni mwa majukumu ya msingi ya Kamati yetu ni kuchambua mapendekezo ya Serikali kuhusu Makadirio ya Wizara husika ya Mapato na Matumizi ya kila mwaka, hivyo katika kutekeleza jukumu hilo lililoelezwa katika Kanuni ya 107(3) Kamati yangu ilikaa na kuijadili na hatimae kupitisha Makadirio ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto na leo hii kwa ruhusa yako na kwa niaba ya Kamati nawasilisha Maoni ya Kamati kuhusiana na Bajeti hiyo.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya utangulizi huo sasa naomba nitekeleze jukumu lililonileta hapa mbele ya Baraza lako Tukufu.

**Mheshimiwa Spika,**

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto kwa mwaka wa fedha **2024/2025** ina fungu **moja (1)** ambalo ni **H04** na imepanga kutekeleza **Programu Kuu Tatu (3) zenye Programu Ndogo Tano (5)** ambapo kwa ujumla fedha zilizoombwa kwa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto ni **Shilingi Bilioni 23,315,462,000 (Bilioni Ishirini na Tatu, Milioni Mia Tatu na Kumi na Tano, Laki Nne Sitini na Mbili Elfu)**.

**Mheshimiwa Spika,**

Bajeti ya wizara hii imepanda kutoka bilioni 9.9 kwa mwaka 2023/2024 mpaka kufikia bilioni 23.3 kwa mwaka 2024/2025 hii ni kutokana na kuwepo kwa mradi wa kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania(PAMOJA) wenye thamani ya bilioni 8.1, ambapo miongoni mwa majukumu yanayokwenda kutekelezwa na Mradi huu ni; Kuwawezesha wanawake kiuchumi, Kupinga na kukabiliana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji wa kijinsia pamoja na Ubunifu na ushirikishwaji.

Hivyo kamati inaishauri Wizara ya fedha kupitia Mradi huu kuupatia fedha kwa wakati na Pia kamati iliitaka Ofisi kuitisha kikao cha Procurement Plan punde tu baada Baraza la Wawakilishi kupitisha bajeti yao ili kuepusha mradi huu kuchelewa kuanza sambamba na kuusimamia vyema utendaji kazi wake ili wapate matokeo mazuri kwenye maeneo yote ya mradi.

## PROGRAMU KUU HIFADHI YA JAMII

**Mheshimiwa Spika,**

Programu hii ya PH0401 inatekelezwa kupitia huduma mbili kuu ikiwemo ya Kutoa huduma Ustawi wa Jamii na Uwendeshwaji wa Pencheni Jamii.

**Mheshimiwa Spika,**

Lengo kuu la kuanzishwa kwa Programu Kuu hii ni kuratibu, kusimamia upatikanaji wa haki kwa makundi yenye mazingira magumu kwa kuimarisha mifumo ya hifadhi ya jamii na huduma kwa wazee, watoto na watu wanaoishi katika mazingira magumu Zaidi ili kupunguza kiwango cha umasikini hapa Zanzibar. Jumla ya asilimia 25 ya bajeti ya wizara imepangwa kutumiwa kwenye fungu kuu hili.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaunga mkono jitihada za Serikali juu ya kuwapatia Wazee makaazi yaliyo Bora ambapo katika Bajeti ya 2024/2025 Serikali kupitia Mradi wa Hifadhi ya Jamii imepanga Kuzifanyia ukarabati nyumba za wazee Sebleni na Limbani. Hivyo, Kamati inaishauri Wizara kusimamia vyema Ujenzi na Ukarabati huo kwa kuwashirikisha wataalamu wa Ujenzi tokea mwanzoni ili kuepusha gharama za ziada. Pia, kamati inaishauri Wizara kuharakisha kumalizia ukarabati wa ukumbi wa mkutano uliopo Sebleni ambao ndio chanzo kikuu cha mapato cha Wizara hii ili kuweza kufikia lengo walilopangiwa la ukusanyaji wa mapato kwani inaonyesha kuwa kwa mwaka uliopita hawakuwa na makusanyo mazuri kutokana na ukumbi huo kuwa mchakavu na unahitaji maboresho.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inatoa pongezi za dhati kwa Mhe. Raisi wa Zanzibar na mwenyekiti wa Baraza la Mapnduzi Mhe. Dkt. Hussein Ali Mwinyi kwa kuongeza kiwango cha Pencheni Jamii kwa asilimia 150 kutoka Shilingi Elfu 20,000 mpaka kufikia Shilingi Elfu 50,000 kuanzia mwezi Julai 2023, hii yote ni kutokana na mapenzi makubwa kwa wazee wetu na wananchi wake kwa ujumla, Hivyo Kamati imeitaka wizara kuratibu vizuri suala la Pencheni Jamii ili kila mzee anayestahili kupata huduma hii aipate kwa wakati tena bila usumbufu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwenye Huduma ya Uwendeshaji wa Pencheni Jamii kwa mwaka 2023/2024 Wizara haikuwa na fungu lolote walilopangiwa na kusababisha huduma hii kutofanyika kwa ufanisi, katika kutekeleza jukumu hilo kwa mwaka wa Fedha 2024/2025 wamepatiwa fungu (HH04010102) ili kusaidia masuala ya uratibu na ufuatiliaji wa pencheni jamii, licha ya kuipatia fungu hili kamati inaishauri Wizara ya Fedha kuiengezea fungu la huduma hii kwa mwaka wa fedha unaofuata ili Wizara iweze kutekeleza majukumu ya huduma hii kwa urahisi na kwa ufanisi kwa maslahi ya wazee wetu.

**Mheshimiwa Spika,**

Kufuatia ziara za kamati kwa familia zenye mazingira magumu, kamati imeishauri wizara kupitia programu ya kutoa huduma ya ustawi wa jamii (HH04010101) kwa kuwapatia kima cha fedha kilichopangwa kwa kila muhitaji na sio kima hicho kwa familia nzima kwa mwezi. Pia kamati imeiomba wizara kuangalia jinsi ya kuwaengezea kima hicho ili kuwapunguzia ugumu wa maisha katika familia hizo.

## PROGRAM KUU YA UTAWALA NA UWENDESHAJI

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa bajeti ya wizara imepangwa asilimia 65 kutumiwa kwenye fungu kuu hili la PH0402. Program hii ina jumla ya program ndogo tatu ambazo ni Utawala na Uwendeshaji; Uratibu wa Mipango, Sera na Utafiti pamoja na Uratibu wa Shughuli za Wizara Pemba.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika fungu la PH0402 limeengezeka kiujumla wake kutoka bilioni 5.6 kwa mwaka 2023/2024 mpaka bilioni 15.1 kwa mwaka 2024/2025 hii ni kutokana na ongezeko la mishahara kwa watendaji, mchango wa serikali wa Bima ya Afya, Mabadiliko ya kada na ongezeko la watendaji kwa Wizara.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati imeitaka Wizara kuwaendeleza watendaji wake kwa masomo ya muda mrefu na muda mfupi hasa kwenye masuala ya unyanyasaji wa kijinsia na masuala yanayohusiana na jamii ili waje wawe msaada kwenye kutoa elimu na kutatua changamoto zinazokabiliana na jamii.

## PROGRAMU KUU YA MAENDELEO YA JAMII NA JINSIA.

**Mheshimiwa Spika,**

Katika utekelezaji wa bajeti ya Wizara zimepangwa asilimia 10 kutumika katika fungu la program kuu hili la PH0403. Miongoni mwa majukumu ya program hii ni kuratibu na kusimamia utekelezaji wa haki za wanawake, wanaume na watoto ikiwa ni pamoja na kusimamia utekelezaji wa sera, sheria zinazohusu maendeleo ya jamii wakiwemo wanawake na watoto pamoja na kuendeleza wanawake hao kwa kuzingatia mipango ya kitaifa,

mikataba ya kikanda na kimataifa.

**Mheshimiwa Spika,**

Kufuatia kikao baina ya Kamati na Wizara, Kamati iliarifiwa kuwa Idadi ya kesi za udhalilishaji zinategemewa kuripotiwa Zaidi kutoka kesi 290 kwa mwaka 2023/2024 mpaka kufikia kesi 400 kwa mwaka 2024/2025 huku ikielezwa miongoni mwa sababu ya engezeko hilo ni elimu na mwamko kwa jamii. Kamati inaishauri Wizara kuendelea kutoa Elimu zaidi juu ya kupiga vita vitendo vya udhalilishaji na jamii kuondoa muhali katika kusaidia kutoa ushahidi ili kuepuka madai ya kesi za udhalilishaji kumalizwa kienyeji na kutofikishwa kwenye vyombo vya sheria.

**Mheshimiwa Spika,**

Kamati inaipongeza Serikali kwa kuanzisha Mahakama zinazohusiana na kesi za udhalilishaji ambazo zitapunguza mkushanyiko wa kesi hiz0 na kurahisisha kutolewa hukumu kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika,**

Mwisho, napenda kuwashukuru na kuwapongeza tena Viongozi na Watendaji wa Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee, na Watoto kwa juhudi wanazochukua katika kutekeleza kazi zao pamoja na ushirikiano wao kwa Kamati hii. Vile vile, nawashukuru sana Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako Tukufu kwa kunisikiliza kwa utulivu wa hali ya juu wakati wote nilipokuwa nikiwasilisha hotuba hii.

**Mheshimiwa Spika,**

Kwa vile Kamati imepitia, imejadili na kuyakubali mapendekezo Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Wizara ya Maendeleo ya Jamii,

Jinsia, Wazee, na Watoto kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Sasa niwaombe Waheshimiwa Wajumbe wa Baraza lako waijadili, watoe ushauri pamoja na mapendekezo yao na hatimae waiunge mkono bajeti hii ili wamuwezeshe Mheshimiwa Waziri kufanikisha na kutekeleza yale waliojipangia katika mwaka wa fedha 2024/2025.

**Mheshimiwa Spika,**

Baada ya kusema hayo machache, Kwa niaba Kamati naunga mkono hoja.

**Mheshimiwa Spika,**

Naomba kuwasilisha.

…………………………………………,

**Sabiha Filfil Thani,**

**Mwenyekiti,**

**Kamati ya Ustawi wa Jamii,**

**BARAZA LA WAWAKILISHI,**

**ZANZIBAR.**